*Check Against Delivery*

# HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA, (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE UZINDUZI WA MIONGOZO YA MAFUNZO KATIKA MAENEO YA KAZI, TAREHE 16 SEPTEMBA, 2017, DODOMA

- Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;
- Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira;
- Waheshimiwa Mawaziri Mliopo hapa;
- Waheshimiwa Wabunge Mliopo hapa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Viongozi wa Serikali mliopo hapa;
- Bwana Eric Shitindi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu;
- Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa;
- Bibi Mary Kawar, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani, Ofisi za Tanzania, Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda;
- Dkt. Aggrey Mlimuka, Mkurugenzi Mtendaji, wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE);
- Dkt. Yahaya Msigwa, Katibu Mkuu, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);
- Waajiri Wote Mliopo Hapa;
- Wawakilishi wa Vikundi na Taasisi za Vijana;
- Wageni Waalikwa;
- Wanahabari;
- Mabibi na Mabwana.

**SHUKRANI**

- Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo ili tushiriki tukio hili muhimu la Uzinduzi wa Miongozo ya Kitaifa ya kusimamia Mafunzo katika Maeneo ya Kazi. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi za Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu pamoja na Mhe. Antony Mavunde, Mbunge wa Dodoma Manispaa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Timu yao ya Wataalamu kwa kuona umuhimu wa kuandaa Miongozo hii ya kusimamia Mafunzo Maeneo ya Kazi katika kipindi hiki ambacho Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza kuimarisha ujuzi wa nguvukazi ya taifa kwa ajili ya kuwezesha ustawi wa uchumi wa Viwanda.

- Kwa upande mwingine, nawashukuru sana wadau wetu kwa kushirikiana na Ofisi yangu kufanikisha utengenezaji wa miongozo hii ambayo tunaizindua leo. Kwa namna ya pekee nimshukuru Bibi Mary Kawar, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Kanda ya Afrika Mashararikil; Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kuhudumia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) pamoja na wadau wetu wa utatu ambao ni Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA). Aidha, niwashukuru pia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF); Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); Bazara la Elimu ya Ufundi (NACTE); Mamlaka ya Mafunzo na Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) kwa michango mbalimbali ya kitaalamu kufanikisha utengenezaji wa miongozo hii.

- Napenda pia kuwashukuru wote mliokubali wito wetu wa kuja kushiriki nasi katika tukio hili lenye umuhimu wa kipekee kwa vijana wetu hususan katika kushughulikia tatizo la ukosefu wa ajira. Tatizo ambalo kwa kiwango kikubwa linasababishwa na ukosefu wa ujuzi na stadi zinazohitajika katika Soko la Ajira, kwa maana ya ujuzi na stadi za kujiajiri au kuajiriwa.

## 1. <u>Malengo ya na Chimbuko la Miongozo</u>

**Ndugu Washiriki,** chimbuko la Miongozo hii ni kutatua tatizo la ukosefu wa ajira nchini kwa kuwa na mafunzo yanayosimamiwa na Serikali. Tunafahamu kuwa Ukosefu wa ajira ni changamoto kubwa kwa sasa duniani ambapo Ripoti ya mwaka 2017 ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), kuhusu hali ya ajira duniani inaonesha kuwa zaidi ya watu **Milioni 201** sawa na **asilimia 5.8** ya watu wanaostahili kufanya kazi hawana kazi. Kati ya Watu hao vijana ni **Milioni 53.5** sawa na **asilimia 13.7.** Kwa upande wa Tanzania, utafiti wa nguvu kazi wa mwaka 2014 unaonesha kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira nchini ni **asilimia 10.3** na kwa vijana ni **asilimia 11.7.**

**Ndugu Washiriki,** utafiti huo unaonesha kuwa takriban **asilimia 79.9** ya nguvu kazi ya taifa ina ujuzi wa kiwango cha chini na **asilimia 20.1** ya nguvu kazi ina ujuzi wa kiwango cha kati au cha juu. Tumeshuhudia katika nyakati tofauti Waajiri wengi wakikiri kushindwa kuwaajiri vijana wakiwemo wenye shahada kutokana na kukosa ujuzi stahiki. Hivyo, Msingi wa kuandaa programu hii ya kukuza ujuzi umetokana na nia ya serikali ya awamu ya tano ya kuhakikisha tunakabiliana na tatizo la ukosefu wa Ajira.

**Ndugu Washiriki,** kutokana na hali niliyoieleza, suala la kuimarisha uwezo wa nguvu kazi ya taifa ni muhimu sana, na njia bora ni kwa kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa kuweka miongozo bora itakayowaongoza wadau wote wakiwemo Serikali, Waajiri, Wafanyakazi na Vijana kutoa Mafunzo. Hivyo, Uzinduzi wa Miongozo hii umekuja katika wakati muafaka.

**Ndugu Washiriki,** Miongozo hii imekusudia kuweka mfumo madhubuti wa kuchochea na kusimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu (internship training) na mafunzo ya uanagenzi (Apprenticeship training). Miongozo hii imelenga kuongeza ari kwa waajiri na wadau wengine kushiriki katika kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi za kazi ili kuhakikisha wahitimu na wanagenzi wanapata stadi za kazi na ujuzi stahiki wa kuajirika au kujiajiri katika soko la ajira. Hali ambayo itachochea ukuzaji wa viwanda na kupunguza ukosefu wa ajira kwa watanzania hususan vijana.

**Ndugu Washiriki**, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoanza kuweka malengo ya ujenzi wa viwanda, mbali na kuwezesha kukua kwa kilimo na kuongeza thamani mazao yetu, pia alilenga kupanua wigo wa ajira za viwandani ambapo kiwanda kinaweza kuajiri watu zaidi ya 1000. Hivyo basi, Miongozo hii itasaidia kuboresha mazingira ya biashara nchini kwa maana ya kuhakikisha taifa lina nguvu kazi yenye weledi wa kutosheleza mahitaji ya soko la ajira hivyo kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya Nchi.

**Ndugu Washiriki,** Serikali imekua ikipokea malalamiko kutoka kwa waajiri ya kwamba wahitimu wengi wa ngazi mbalimbali za mafunzo wanaingia katika soko la ajira wakiwa hawana ujuzi unaohitajika na hivyo waajiri kulazimika kutafuta wafanyakazi kutoka nje ya nchi. Jambo hili tulilijadili kwa pamoja yaani Serikali, Waajiri na Wafanyakazi na kukubaliana kuwa kuna haja sasa ya kuhakikisha tunachochea na kuimarisha mfumo wa utoaji mafunzo yanayo-fanyika maeneo ya kazi. Na kwa pamoja tuliazimia kuandaliwa kwa Miongozo ya Kitaifa ya kusimamia mafunzo ya vitendo kwa wahitimu (internship guidelines) na mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship guidelines); lengo ni kuhakikisha mafunzo yatolewayo maeneo ya kazi yana ubora unaohitajika.

vya umma na binafsi. Aidha, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka huu wa fedha (2017/2018) Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya kukuza ujuzi kwa Vijana ili kuhakikisha tunaziba pengo la ujuzi na stadi mbalimbali za kazi.

**HITIMISHO**

**Ndugu Washiriki,** kama nilivyoeleza awali Miongozo nitakayo-izindua leo inalenga kuwezesha utekelezaji wa programu za kukuza ujuzi nchini hususan kupitia mafunzo ya vitendo kwa wahitimu (internship) pamoja na mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship). Miongozo hii ni ya kitaifa na hivyo imekusudiwa kutumika kwa wadau wote nchini wanaojihusisha na utekelezaji wa programu mbalimbali za mafunzo ya uanagenzi pamoja na mafunzo ya vitendo kwa wahitimu. Serikali inatambua na kuthamini michango na juhudi za wadau wote hususan Asasi za kiraia, sekta binafsi, Taasisi za Mafunzo, Taasisi za Kimataifa pamoja na Wadau wa Maendeleo katika kuwezesha vijana wa kitanzania kujiajiri na kuajirika.

**Ndugu Washiriki,** nimetaarifiwa kuwa wapo waajiri na tasisi za mafunzo ambazo pamoja na kutokuwepo kwa miongozo wameshaanza kutoa mafunzo ya Uanagenzi na ya vitendo kwa wahitimu. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana kwa moyo mnaouonesha katika kuwasaidia vijana wetu. Naomba pia niwahakikishie kuwa Serikali itaendelea kushirikiana nanyi kuhakikisha tunaimarisha uwezo wa nguvu kazi ya taifa.

**Ndugu Washiriki,** Wito wangu kwa wadau ni kuendelea kutekeleza programu za kukuza ujuzi sambamba na kutumia miongozo hii. Aidha, napenda nichukue fursa hii pia kuomba vyombo vya habari vikiwemo redio, Televisheni, Magazeti na mitandao ya kijamii kuhamasisha umma wa Watanzania na wadau wote kushirikiana nasi katika kutekeleza programu ya kukuza ujuzi.

**Ndugu Washiriki,** kabla ya kuhitimisha naomba nirudie kuwapongeza tena wadau wote walioshiriki katika kuandaa miongozo hii muhimu na pia wote mliokubali mwaliko wetu kuja kushiriki katika uzinduzi wake. Niwashukuru pia wote walioshiriki katika maandalizi ya tukio hili na kutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo. Matengemeo yetu ni kwamba Waajiri, Vijana, Wafanyakazi, na taasisi za Mafunzo mtatumia miongozo hii kama chachu ya kuleta mapinduzi ya ujuzi nchini na hivyo kuhakikisha taifa linakua na nguvu kazi yenye weledi wa kutosha.

**Ndugu Washiriki, Mabibi na Mabwana,** baada ya kusema hayo machache napenda nitumie nafasi hii kuwatakia utekelezaji mwema wa miongozo hii, na naomba sasa nitamke kuwa **Mwongozo wa Mafunzo ya Uanagenzi na Mwongozo wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu** imezinduliwa Rasmi kwa Matumizi.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**